



- Funza akidondoka chini hana uwezo tena wa kupanda kwenye mti au kufanya uharibifu.

1. Buu

- Buu walio ndani ya gamba, wanaweza kuuawa kwa kutumia ncha kali, kama vile spoku ya baiskeli, ili kuwatoboa wakiwa ndani ya mashimo.

2. Kifa Uwongo

- Muue Kifa uwongo kila unapomwona

Angalizo

Kata na choma moto mikorosho yote iliyoshambuliwa na ambayo haina dalili ya kuchipua



Mkorosho uliokufa kwa mashambulizi ya kifauongo



KUDHIBITI KIFA UWONGO KATIKA MIKOROSHO



Kimetayarishwa na:

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S. L. P. 509,
MTWARA
Email : cdnaliendele@tari.go.tz

April 2019

KIFA-UWONGO.

1.0 Utangulizi

Kifa uwongo ni mdudu aina ya kifukuzi ambaye hushambulia mashina ya mikorosho. Mashambulizi yanapozidi huweza kuua mkorosho wote. Jina Kifa uwongo limetokana na mbinu yake ya kujifanya amekufa mara anapohisi hatari. Baada ya dalili ya hatari kuondoka huendelea na shughuli zake kama kawaida.

2.0 Sifa na maisha ya Kifa uwongo

- Kifa uwongo kamili aliyekomaa, ana rangi ya kahawia na urefu wa sentimita mbili
- Ana mdomo mrefu uliochongoka ambao daima anauficha kwa kuulaza kifuani.



Kifauwongo kamili

- Mzunguko wa maisha ya Kifa uwongo hupitia hatua za yai, funza, buu na mdudu kamili.

- Funza huwa mweupe, mwenye ngozi ya kukunjamana na kichwa cha rangi ya kahawia iliyokolea na daima huonekana amejikunja



Funza wa kifauwongo

- Kifa uwongo jike hutoboa gamba la mkorosho kwa kutumia mdomo na hutaga yai moja moja katika sehemu tofauti alizotoboa
- Mayai huanguliwa na kuwa funza ambao hushambulia gamba la mkorosho kwa kupekecha kwa kutumia mdomo
- Kifa uwongo kamili ana mabawa na anaweza kuruka.

3.0 Dalili za mashambulizi

- Matundu katika shina la mkorosho yanayotoa mchanganyiko wa utomvu na takataka kama maranda ya mbao

- ambayo hatimaye hugeuka rangi na kuwa meusi.



Mashambulizi ya kifauwongo kwenye shina

- Majani ya mkorosho uliyoshambuliwa sana, hubadilika na kuwa njano, kisha hunyauka na hatimaye hukauka.

4.0 Kudhibiti Kifa uwongo

1. Funza

- Fanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa kila mkorosho ili kubaini dalili za mashambulizi
- Dalili za mashambulizi zinapoonekana bandua gamba katika sehemu iliyoshambuliwa kwa kutumia kisu au panga na kuwaondoa funza wote.